







Khalai azungumza na mimea

Khalai talks to plants

-  Ursula Nafula
-  Jesse Pietersen
-  Ursula Nafula
-  Kiswahili / English
-  Level 2

(imageless edition)






Khalai ni msichana mwenye umri wa miaka saba. Jina lake lina maana ya 'aliye mzuri' katika lugha yake ya Lubukusu.

...


This is Khalai. She is seven years old. Her name means 'the good one' in her language, Lubukusu.



Khalai anaamka na kuongea na mmea mchanga wa Mchungwa, “Tafadhali mti wa Mchungwa, kua mkubwa uzae machungwa mengi mabivu.”

...


Khalai wakes up and talks to the orange tree. “Please orange tree, grow big and give us lots of ripe oranges.”



Khalai anaenda shuleni na njiani
anaongea na Nyasi, “Tafadhali
Nyasi, kua kijani zaidi na zaidi na
wala usikauke.”

...


Khalai walks to school. On the way
she talks to the grass. “Please
grass, grow greener and don’t dry
up.”



Khalai anayapita Maua ya mwituni
na kusema, “Tafadhali Maua,
endelea kunawiri ili niweze
kukuweka kwenye nywele zangu.”

...


Khalai passes wild flowers. “Please
flowers, keep blooming so I can
put you in my hair.”



Akiwa shuleni, Khalai
anazunguumza na Mti ulioko
katikati ya shule, “Tafadhali Mti,
toa matawi makubwa ili tusome
chini ya kivuli chako.”

...


At school, Khalai talks to the tree in
the middle of the compound.
“Please tree, put out big branches
so we can read under your shade.”



Khalai anazunguumza na ua unaoizingira shule yake, “Tafadhali ua, kuwa mwenye nguvu ili uzuie shule yetu kutokana na watu wabaya.”

...

Khalai talks to the hedge around her school. “Please grow strong and stop bad people from coming in.”



Anaporudi nyumbani alasiri, Khalai
anautembelea mti wa Mchungwa
kuangalia kama machungwa
yameiva.

...

When Khalai returns home from
school, she visits the orange tree.
“Are your oranges ripe yet?” asks
Khalai.

“Machungwa bado mabichi,”
Khalai anashusha pumzi.

“Nitakuona kesho, we mti wa
machungwa. Labda utanipa
chungwa bivu wakati huo.”

...

“The oranges are still green,” sighs
Khalai. “I will see you tomorrow
orange tree,” says Khalai. “Perhaps
then you will have a ripe orange
for me!”



Storybooks Canada

storybookscanada.ca

Khalai azungumza na mimea

Khalai talks to plants

Written by: Ursula Nafula

Illustrated by: Jesse Pietersen

Translated by: (sw) Ursula Nafula

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by Storybooks Canada in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/).